

NAMBARI YA MTAHINIWA _____

SMZ

BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

MTIHANI WA DARASA LA NNE

121

KISWAHILI

MUDA: SAA 2.00

JUMATATU 25 NOVEMBA, 2019 MCHANA

MAAGIZO KWA WATAHINIWA

- 1. Mtihani huu una sehemu NNE (4) A, B, C na D.**
- 2. Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A na B. Swali MOJA (1) kutoka sehemu C na swali MOJA (1) kutoka sehemu D.**
- 3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.**
- 4. Majibu YOTE yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.**
- 5. Majibu YOTE yaandikwe kwa kalamu ya buluu au nyeusi.**

KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI

| NAMBARI YA SWALI | ALAMA | SAINI |
|-------------------------|--------------|--------------|
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | | |
| 6. | | |
| 7. | | |
| 8. | | |
| 9. | | |
| 10. | | |
| JUMLA | | |

Mtihani huu una kurasa 13 zenyе maandishi

Ukurasa wa 1 kati ya 13

SEHEMU A: (Alama 20)

UFAHAMU

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata.

Sungura aliwadanganya wenzake kwa kipindi kirefu. Alitumia ujanja wake kuwafanya wenzake wajinga. Alisababisha wengi wapigwe na wakati mwengine hati kupoteza maisha. Siku moja wanyama waliitisha mkutano ili kila mmoja atoe malalamiko yake. Katika mkutano wao, wanyama wote walikubaliana kumkomesha sungura kwa ujanja wake.

Mnyama aliyeseka zaidi alikuwa ni fisi ambaye alidanganywa kwamba mkono wa binadamu ungeanguka. Mara nyingi fisi alimfuata binadamu lakini aliambulia kipigo cha kumvunja mbavu. Fisi alipata majeraha makubwa kutokana na kipigo alichokipata. Wanyama wote walimsikitikia sana fisi.

Zaidi ya hayo, sungura hakuwa na mashirikiano mazuri na wenzake, alikataa kushiriki katika kazi ya uchimbaji wa kisima cha maji na badala yake akaendelea kuiba maji msimu wa ukame. Wanyama wote kwa pamoja waliamua ni heri sungura afe. Fisi, chui na simba waliahidi kuongoza msafara mpaka wamtie sungura mikononi.

1. **Maswali**

i. Kwa kipindi gani sungura aliwadanganya wenzake?

ii. Sungura alitumia ujanja wake kwa lengo gani?

iii. Bainisha tabia mbili (2) mbaya alizokwanazo sungura.

iv. Wanyama waliamua nini katika mkutano wao?

v. Unadhani kwa nini wanyama wote walimsikitikia sana fisi?

2. Toa maana ya neno au kifungu cha maneno kilichopigiwa mstari.

SEHEMU B: (Alama 40)

SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

3. Ainisha maneno yaliyopigiwa mstari.

Kwa mfano:

- i. Mwizi amekamatwa.
N _____

- ii. Yule ndiye mkorofsi.

iii. Mwanafunzi hodari amepewa zawadi.

iv. Wewe ni rafiki yangu.

v. Ameruka mara tatu.

vi. Watoto wote wanasoma vizuri.

4. Toa kinyume cha maneno yafuatayo:
Nambari moja imetumika kama mfano.

| | NENO | KINYUME |
|------|-------------|----------------|
| i. | Nenda | Rudi |
| ii. | Mbovu | |
| iii. | Rafiki | |
| iv. | Cheka | |
| v. | Amani | |
| vi. | Funga | |

5. a) Andika nambari zifuatazo kwa maneno.

- i. 1,100

- ii. 98,888

- iii. 362,045

b) Andika maneno yafuatayo kwa nambari.

- i. Elfu moja na arubaini na mbili.

- ii. Laki nne, elfu hamsini, mia tano na hamsini na tano.

6. a) Andika sentensi zifuatazo kwa lugha ya Kiingereza.

- i. Bendera yetu ina rangi nzuri.

ii. Embe na ndizi ni matunda matamu.

iii. Tulinunua vijiko kumi na nane na uma mmoja.

b) Eleza umuhimu wa vitu vifuatavyo:

i. Chandarua

ii. Miti

SEHEMU C: (Alama 20)

FASIHI

Jibu swali MOJA (1) tu katika sehemu hii.

7. Tunga hadithi fupi inayotoa ujumbe "Umoja ni Ushindi".

NAMBARI YA MTAHINIWA _____

8. a) Eleza mafunzo ya methali zifuatazo:

i. Mtaka cha mvunguni sharti ainame.

ii. Usipoziba ufa utajenga ukuta.

iii. Mwenda pole hajikwai.

b) i. Nini maana ya ngonjera?

ii. Orodhesha vipengele vinne (4) muhimu vya ngonjera.

SEHEMU D: (Alama 20)

UTUNGAJI

Jibu swali MOJA (1) tu katika sehemu hii.

9. Andika kadi ya mwaliko kwa rafiki yako, umualike katika sherehe ya maulid ya kuzaliwa kwa ndugu yako.

NAMBA RI YA MTAHINIWA _____

10. Taja vipengele vyote muhimu vya uandishi wa barua ya kawaida.

NAMBA RI YA MTAHINIWA _____

=====